Mtandao wa Wakulima Wadogo wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAFF)
na
Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA)

# KITINI CHA SERA – NA. 1/2016



# *Bajeti Tuitakayo Kwa Mwaka 2016/17 na Baadaye*

## UCHAMBUZI WA BAJETI YA SEKTA YA KILIMO - TANZANIA

# Uchambuzi wa Bajeti Sekta ya Kilimo 2015/16
# *UWEKEZAJI WA KIMKAKATI: FUNGU KUBWA BAJETI YA MAENDELEO KULIKO MATUMIZI YA KAWAIDA?*

## 1. Utangulizi

Serikali ya Awamu ya Tano, imeanza kazi katikati ya utekelezaji wa mwaka wa bajeti 2015/16. Katika uteuzi wa watendaji wakuu wa wizara hasa mawaziri, serikali imepunguza idadi ya wizara kutoka 30 hadi 19. Mabadiliko haya yameigusa Wizara ya Kilimo, Usalama wa Chakula na Ushirika, kwa kuiunganisha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Wizara nyingine zinazohusika na Kilimo ni pamoja na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Pia zipo wizara kama ile ya Ardhi na Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Kazi, Usafirishaji na Mawasiliano nazo zinagusa kilimo kwa namna tofauti. **Kwa maana nyingine mafanikio ya sekta ya kilimo yanategemea sana namna wizara nyingine zinavyoungamanishwa na ufanisi wa kisekta.**

### 1.1 *Chanzo cha Takwimu kwenye Kitini hiki*


Mapitio ya machapisho mbali mbali yalifanywa katika kupata takwimu sahihi. Machapisho hayo ni pamoja na hotuba ya Waziri Mkuu Mstaafu Mh. Mizengo Kayanza Pinda aliyoitoa kwenye Bunge la Tanzania, tarehe 12 Mei 2015, Vifungu vikubwa vya bajeti namba 43, 24 na 05 (Wizara ya Kilimo), 56 cha TAMISEMI 99 (Mifugo na Uvuvi) vilipitiwa ili kuboresha takwimu hizi. Pia mapitio kwenye bajeti zilizopita yalifanywa ili kuleta ulinganifu. Taarifa kuhusu baraza la mawaziri zinapatikana kwenye tovuti ya www.ikulu.go.tz.

### 1.2 *Kitini hiki kinalenga nini*

Kitini hiki kimeandaliwa ili kukuza uelewa wa wadau mbalimbali kuhusu utengaji wa fedha kimkakati kwenye za Kilimo. Wadau wa sekta ya Kilimo ni kama vile wakulima wadogo, wabunge, watunga sera na watoa maamuzi pamoja na sekta binafsi. Aidha Kitini kinalenga kuchambua changamoto za mgawanyo wa rasilimali (fedha za umma) katika kutatua changamoto za uhaba wa chakula na kupunguza umasikini Tanzania.


## 2. Malengo ya Kubadilisha Kilimo: Ni halisia kiasi gani?

Ili kutengeneza ajira, kuongeza uzalishaji na tija katika jitihada za kuondoa njaa na umasikini, Serikali imekuwa ikitenga fedha na kuwekeza kwenye sekta ya kilimo. Bila kuangalia uwiano wa mfumuko wa bei, mamlaka husika zimeendelea kuongeza na kupitisha fungu la bajeti ya kilimo kilimo kila mwaka. Hata hivyo kuna tofauti kubwa kati ya bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha fedha halisi zinatopatikana na kugawiwa kwenye sekta ya kilimo. **Kwa kipindi cha miaka mitatu mfulilizo, bajeti halisi ya maendeleo inayopatikana imekuwa chini ya nusu (50%) ya bajeti iliyopitishwa na kuidhinishwa**. Hii ni kinyume na matarajio ya wakulima wadogo. Madhalani, katika mwaka wa fedha 2014/15, hadi kufikia mwisho warobo ya tatu ya mwaka, Wizara ya Kilimo ilikuwa imepokea takribani robo tu (yaani 25%) ya bajeti iliyoidhinishwa kwa shughuli za maendeleo.




### 2.1 ***Wizara ya Kilimo kama Kielelezo cha Kipaumbele cha Matumizi: Je Tanzania hutenga 10%?***

Ufanisi kwenye sekta ya kilimo hutegemea Wizara ya Kilimo pamoja na wizara nyingine. Hata hivyo jumla ya fedha zinazotengwa imeendelea kushuka ikilinganishwa na kipimo cha mfumuko wa bei. Takwimu zilizoko hapa chini zinaonesha bajeti iliyopitishwa kati ya mwaka 2010 na 2014 hakukuwa na uwiano wa ongezeko la bajeti na ukuaji wa sekta ya kilimo. Ukuaji wa sekta ya kilimo umebakia kwenye wastani wa 4% kwa mwaka. Kwa miaka kadhaa, utekelezaji wa makubaliano ya kuendeleza Kilimo ya Bara la Afrika (CAADP) kupitia Azimio la Maputo mwaka 2003 na Azimio la Malabo 2014, Tanzania imekuwa chini ya lengo la kutenga 10% ya bajeti ya taifa. Kwa mwaka 2014/15, kilimo ilitengewa kiasi cha 5.5% ya bajeti kuu.




Katika chati inayoonesha bajeti kati ya mwaka 2010 -2015, mtiririko wa bajeti unaonesha kuwa fungu la Wizara ya Kilimo, lilikuwa na ukuaji wa wastani. Hata hivyo kiwango cha fedha zinazotengwa cha bajeti ya maendeleo ni kidogo mno ili kuleta mabadiliko yanayokusudiwa katika sekta ya kilimo. Bajeti ya Kilimo imeongezeka kutoka Shilingi 52 bilioni (2.95% ya bajeti) mwaka 2001/02 hadi Shilingi 1.084 trilioni (5.5%) mwaka 2014/15. Hata hivyo bado fungu hili liko chini ya lengo la Malabo la asilimia 0 (10%).

- Pamoja na ongezeko la kiasi cha fedha zinazotengwa kila mwaka, ukuaji wa sekta ya kilimo kwa mwaka umeendelea kuwa chini ya asilimia nne (4%), isipokuwa kwa mwaka wa fedha 2004/05. Lengo la Malabo ni kukuza kilimo kwa silimia 6 (6%) kwa mwaka.

**Je tatizo ni nini?**

- Isipokuwa kwa mwaka 2003/4 na 2004/05, fungu la bajeti kwa matumizi ya maendeleo lilikuwa kubwa kuliko matumizi ya kawaida. Na hii ndiyo miaka pekee ambayo kilimo kimekua kwa zaidi ya 5%.

### 2.2 **Ulinganifu wa Bajeti: Maendeleo na Kawaida**

- Je ni vitu gani vya kuzingatia kwenye bajeti? Je ni bajeti iliyotengwa na kupitishwa,

au kiwango cha fedha kilichopatikana na kutumika vizuri? **Hata hivyo uzoefu unaonesha changamoto katika upatikanaji wa fungu la maendeleo la bajeti, ambalo hutumwa kwa kuchelewa, kutengewa matumizi mengine na hata wakati mwingine kukosekana kabisa.** Hali hii ni tofauti na fungu la matumizi ya kawaida katika mwaka husika wa fedha.

## 3. Vyanzo vya Fedha: Je, Pesa hutoka wapi?

Serikali hugharamia fungu la matumizi ya kawaida, ambalo kawaida ni kubwa kuliko la maendeleo. Sehemu kubwa ya fungu la maendeleo huchangiwa na wahisani. Hata hivyo baada ya kukamilisha Mpango wa Kwanza wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP 1), mchango wa wahisani umeshuka kutoka shilingi 105 bilioni mwaka 2012/13 hadi TZS 22 bilioni ilipofikia mwaka 2014/15). Jambo hili ni kiashiria cha umuhimu wa serikali kutenga bajeti toka vyanzo vyake vya ndani badala ya kutegemea wahisani.

- Kama sehemu ya ushirikiano, wahisani wameendelea kufadhili sekta ya kilimo kwa pamoja (basket fund) au kufadhili mradi mmoja mmoja.
- Hata hivyo utegemezi mkubwa kwa wahisani unaweza kuhatarisha uwezo wa kimaamuzi na uendelevu wa miradi husika. Hivi sasa ipo miradi mingi ya umwagiliaji pamoja na vituo vya rasilimali vya Kata ambayo imetelekezwa kutokana na kupungua au kukosekana kwa fedha kutoka kwa wafadhili kabla miradi haijakamilika. Hii ni gharama za uwekezaji ambazo ni vigumu kuzirejesha endapo miradi hiyo haitakamilishwa.
- Kupungua kwa fedha za wahsani kunahusishwa zaidi na kufikia ukomo wa ASDP1- mfumo ambao ulikuwa unatumia fedha za pamoja kwenye kapu (basket fund) .





## 4. Vipaumbele kwenye fungu la Maendeleo la Bajeti 2014/15

### *4.1 Kwa kiwango gani uwekezaji ni wakimkakati?*

Tanzania hujitosheleza kwa chakula kwa kiwango kikubwa. **Pamoja na kuwa na hekta milioni 29 ambazo zinaweza kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji, kiwango kilichojengewa miundo mbinu hiyo ni chini ya hekta laki tano**. Ruzuku ya mbolea hutumia sehemu kubwa ya bajeti kwa miradi iliyotengwa (earmarked) katika Wizara ya Kilimo Tanzania. Katika fungu la maendeleo, kwa mwaka wa fedha 2015/16, maeneo kadhaa yamepewa kipaumbele, ikiwa ni pamoja na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa au BRN, Upatikanaji wa ruzuku za pembejeo (mbolea, mbegu na viuatilifu), Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (NFRA) na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko.

Matarajio ni kuwa, uwekezaji huu utachangia kuleta mabadiliko ya sekta na kuimarisha usalama wa chakula na kuondoa umasikini. Hata hivyo, takwimu na shuhuda ziliopo zinaonesha utekelezaji mdogo, usimamizi dhaifu wa fedha hasa kwenye uendeshaji wa Wakala wa Hifadhi




ya Chakula wa Taifa na usimamizi wa mifumo ya ruzuku kwa viuatilifu, mbegu na mbolea.

Kiasi cha 36% ya bajeti ya maendeleo kwa wizara ya kilimo kwa mwaka wa fedha 2015/16 kilitengwa kutumika kwenye shughuli za Wakala wa Hifadhi ya Chakula na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Fungu la kuendeleza umwagiliaji na miundombinu ya maghala (ukarabati chini ya Matokeo Makubwa Sasa na Ukanda wa SAGCOT) zimetengewa kiasi cha 6% ya bajeti ya maendeleo kwa mwaka husika. Ikumbukwe pia, pamoja na kwamba kiasi kikubwa cha fedha zimetengwa kwa ajili ya Wakala wa Chakula na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, mwaka huo wa fedha unafuatia mwaka wa mavuno mengi wa 2014/15. Bila shaka kuna umuhimu wa kuangalia fedha hizo ili kuandaa mfumo bora wa masoko, uhifadhi na uchakataji wa mazao ili kujenga mnyororo thabiti wa thamani ya mazao unaowajumuisha wajasiriamali wanawake na vijana na kukuza ushindani wa kununua mazao. Kimsingi, fedha nyingi zilitengwa kuboresha miundo mbinu ya umwagiliaji chini ya BRN na katika uwekezaji mkubwa kwenye eneo la ukanda wa SAGCOT, bila kuwa na mkakati madhubuti wa kushughulikia halmashari zinazokabiliwa na njaa kila mwaka. Uwiano huu wa kuwekeza kwenye maeneo fulani fulani unaziweka wilaya za pembezoni na zenye ukame kuwa kwenye wakati mgumu kwa suala la usalama wa chakula.

Licha ya jitihada za kuwekeza rasilimali za umma kwenye maeneo mbalimbali, tafiti zilizopita zinatoa hadhali kuhusu baadhi ya vipaumbele hivyo kama ifuatavyo:


- Kuwepo udhaifu katika usimamizi wa ruzuku za pembejeo (mbegu, viuatilifu na mbolea) umekuwa na matokeo mchanganyiko kuliko matarajio miongoni mwa wakulima wadogo.
- Kutotengewa bajeti kwa juhudi za uzalishaji mbegu kupitia daraja la kuazimiwa (QDS) kupitia wakulima wadogo kunaathiri tija na kuhatarisha usalama na uhakika wa mbegu bora nchini.
- Kushindwa kupima na kurasimisha ardhi ya kilimo kutokana na bajeti ndogo imekuwa ni mojawapo ya sababu za migogoro isiyoisha baina ya wawekezaji, wafugaji na wakulima wadogo.
- Kutenga fungu kubwa la bajeti kwa shughuli za Wakala wa Chakula na Bodi ya Nafaka kunaweza kudumaza jitihada za kujenga minyororo ya thamani na uchakataji katika kuimarisha sekta ya wajasiriamali wadogo na sekta binafsi za wazalendo nchini. Mchango wa sekta binafsi ni wa muhimu sana kwenye minyororo ya thamani na kupanua ajira.

### *4.2 Bajeti ya Maendeleo 2015/16*

- Katika bajeti ya maendeleo kwa mwaka 2015/16, fungu Na 5 (umwagiliaji) imechukua 59% ya Shilingi 211 bilioni zilizotengwa kwa idara na taasisi mbalimbali.
- Fungu Na 24 ambalo ni la muhimu katika kuongeza uzalishaji na tija pamoja na uendelezaji wa vyama vya wakulima na ushirika halijatengewa fedha. Hii inatishia uimara wa taasisi za wakulima na kuendeleza utegemezi kwa serikali kwenye shughuli za uzal-

ishaji na masoko ya mazao ya wakulima. Kwa mwaka 2015/16 fungu la ushirika halikutengewa fedha zozote za maendeleo.

- Kwa kiwango kidogo pia, fedha kiasi zimetengwa kuendeleza Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Wakala wa Chakula wa Taifa, TAMISEMI, na uendelezaji wa mifugo na uvuvi pamoja na biashara kwenye vifungu mbalimbali vya bajeti




## 5. Wakulima wadogo, Vijana na Wanawake kwenye Bajeti ya 2015/16?

Fungu la bajeti linalolenga uwekezaji kwenye shughuli zinazonufaisha vijana na wanawake linaweza kuchambuliwa kwa mtizamo mpana na miradi mbalimbali. Kwenye ngazi za halmashauri yapo maagizo ya kutenga walau 5% ya pato lao la ndani kwa kulenga vijana na wanawake. Pia halmashauri zinayo maagizo ya kutenga walau hekta 10,000 kusaidia miradi ya kilimo ya vijana. Hata hivyo kutokana na usimamizi hafifu wilaya nyingi zimekuwa hazijatekeleza maagizo haya.

Kwa kiasi kikubwa, makundi ya vijana na wanawake hayaonekani kupewa kipaumbele kwenye bajeti, bali imetengwa kiujumla. Ni bora zikaweko jitihada za makusudi kuhakikisha makundi haya yanaonekana kwenye mafungu ya bajeti. Hakuna mipango wazi kwa sasa hususani kwa mwaka wa fedha 2015/16.

## 6. Mapendekezo Kuhusu Bajeti rafiki kwa Wakulima wadogo mwaka 2016/17

(i) Kwa kuwa kuna tofauti kubwa kati ya bajeti iliyotengwa, iliyopitishwa na fedha zilizopatikana na zilizotumika, upo umuhimu wa kufanya uchambuzi kuhusu vyanzo vya mapato (vipya na vya zamani) na kuweka mfumo utakaozuia/punguza uvujaji wa mapato. Halmashauri zijengewe uwezo kuhakikisha zinakusanya mapato baada ya kubainisha vyanzo, na inapo wezekana zinaweza kuingia ubia na sekta ama makampuni binafsi kutekeleza shughuli za maendeleo. Kwa mwaka 2015/16, bajeti ya maendeleo ilitegemewa kutoka vyanzo vya ndani (35%) na kutoka kwa wahsani (65%) kama ruzuku na mikopo ya masharti nafuu. Wahisani wanaweza kuwa na malengo tofauti, na nchi haiwezi kuendelea kuwategemea, kwa hiyo kuna umuhimu wa kupunguza utegemezi kwa wafadhili kwenye bajeti yetu;

(ii) Pamoja na kuwa Tanzania imezingatia uwekezaji na kulenga kukuza kilimo kwa 6% kwa mwaka kama yalivyo makubaliano ya CAADP, tatizo kuwa liko kwenye upatikanaji wa fedha zilizopitishwa na vyombo husika, kama bunge. Kwa mwaka wa fedha 2014/15 na 2015/16, bajeti ya kilimo hajazidi 6% ya fedha zote zilizotengwa kitaifa;

(iii) Mafungu mahsusi kama vile bajeti ya utafiti lazima yaongezwe kufikia walau 1% ya pato kama lilivyokuwa lengo la serikali ya awamu ya nne na kulingana na

makubaliano ya nchi za Afrika kuhusu uwekezaji kwenye utafiti;

(iv) Tafiti za karibuni zinaonesha kuwa mmoja katika watu watatu (theluthi) ya walengwa wa pembejeo za ruzuku ndiyo wamenufaika na mfumo huu. Kuna umuhimu wa kufanya mapitio ya mfumo wa ruzuku na kuhakikisha unanufaisha walengwa kwa wakati;

(v) Ili kupunguza utengemezi wa pembejeo kutoka nje, ni bora kuimarisha sekta ya uzalishaji mbegu ya wakulima wadogo (QDS) na kusaidia kukua kwa wakulima na makampuni binafsi ya kizalendo yanayozalisha mbegu ili kuzalisha mbegu na kuzisambaza badala ya kujikita kutegemea makampuni makubwa ya mbegu kutoka nje;

(vi) Kwa kiasi kikubwa, kama ilivyosemwa hapo kabla, bajeti ya mwaka 2015/16 imeegemewa sana kwenye maeneo ya Matokeo Makubwa sasa na SAGCOT. Mikoa hiyo haiwakilishi nchi nzima, japo huzalisha chakula kingi. Serikali ijenge mifumo ya kusaidia mikoa masikini na yenye upungufu wa chakula kama Shinyanga, Simiyu, Lindi na Mara. Kimsingi kwa bajeti ya 2016/17 kuna haja ya kuchambua mikoa iliyoko pembezoni kuangalia uwezo wake kusafirisha chakula ama kuuza chakula kwa nchi jirani kama sehemu ya mkakati wa kuimarisha biashara za Kilimo;

(vii) Vivyo hivyo, **kuna ulazima wa kufanya mapitio kuhusu mgawanyo wa maafisa ugani uendane na fursa za mikoa husika** ikiwa ni pamoja na kuhakikisha maofisa wameelimishwa vyema na wana vitendea kazi muhimu na maslahi bora;

(viii) Mfumo wa sasa wa bajeti hautoi mwanga na ufafanuzi wa kiasi gani makundi maalum hasa wakulima wadogo, wanawake na vijana yamehusishwa na mahitaji yao kuzingatiwa. Inapendekezwa bajeti iwe wazi kwa jinsi gani mahitaji ya makundi hayo yamezingatiwa;

(ix) Uwepo wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ulenge kutoa elimu na kukidhi matarajio ya wakulima wadogo hususani vijana na wanawake nchini kote hasa vijijini, katika upatikanaji wa mitaji ili kuwekeza kwenye Kilimo;

(x) Japokuwa sekta ndogo za mifugo na uvuvi zinategemewa na watu zaidi ya milioni nne (4), kiasi cha bajeti kinachotengwa ni kidogo sana. Kwa mwaka 2013 kulikuwepo na zaidi ya wavuvi wadogo wapatao 183,341waliokuwa wanajishughulisha na kazi za uvuvi. Tanzania ni miongoni mwa nchi tatu kubwa barani Afrika zenye idadi kubwa ya mifugo. Ipo haja ya kutenga bajeti zaidi kuimarisha sekta hizi ili kuongeza tija, uzalishaji na kupunguza bei za vitoweo ili kuimarisha afya hususani za watoto.

(xi) Kwa kuwa bajeti ya matumizi ya kawaida imekuwa inapatikana bila shida, kuna umuhimu wa kusaidia halmashauri kupata fedha za bajeti ya maendeleo sambamba na ile ya matumizi ya kawaida. Hii inawezekana endapo upelekaji wa fedha za fungu la maendeleo unafanyika wakati ule wa kuhamisha fedha za matumizi ya kawaida, na ifanyike kwa wakati kupitia hazina kuu. Kwa sehemu ambazo kuna upungufu wa bajeti, halmashauri zizingatie kuingia ubia na asasi za kiraia (NGOs) au sekta binafsi. Hili linaweza kuchukua muda kutokana na ukosefu wa uzoefu wa ufanyajikazi pamoja, lakini hatimaye linaweza kuleta matokeo mazuri. Kwa kuanzia, halmashauri zinaweza kuanza kuandaa mijadala ya pamoja kwa kushirikiana na sekta binafsi na asasi za kiraia ili kuondoa mashaka miongoni mwao.

(xii) Uratibu madhubuti ni mojawapo ya vigezo vya mafanikio katika kuleta mabadiliko ya kisekta. Uratibu kwa taasisi za umma unahitajika ili kuleta matokeo mazuri, ya kudumu na makubwa miongoni mwa wadau wanaoshirikiana. Uratibu ni lazima ulenge kuimarisha ushiriki wa makundi madogo kama wanawake, wakulima wadogo na vijana. Taasisi imara za umma zenye uwezo wa kujisahihisha ni muhimu

katika kutengeneza bajeti zenye mtizamo wa kikanda hasa kwenye viwanda kwa kujenga mazingira ya wawekezaji na wadau wengine kwa ujumla wao.

(xiii) Kukamilika kwa miradi kadhaa ya umwagiliaji kama ule wa skimu ya Rudewa wilayani Kilosa na Skimu ya Buhangaza - Muleba ili unufaishe wananchi baada ya ta takribni miaka 7 tangu ianze kujengwa. Mradi wa Rudewa ulitangazwa mwaka jana 2015/16 katika hotuba ya Waziri wa Kilimo kwa Bunge kuwa umekamilika na kuwa unanufaisha watu 3,500, wakati haujakamilika.

(xiv) Ardhi - Kuna umuhimu wa kufanya sensa kubwa ya kupima ardhi kote nchini ili kuwa na mfumo mzuri wa utengaji wa maeneo ya ardhi ili kupunguza migogoro ya ardhi nchini. Aidha zoezi hilo liendani na kuhakikisha umilika sawa wa ardhi kwa wanawake na vijana.





## Usuli Kuhusu ESAFF

ESAFF ni Jukwaa la Wakulima Wadogo wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika linalolenga kupunguza umasikini, athari na njaa kupitia ushawishi wa kisera za kilimo na kwenye mfumo wa bajeti katika ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika. ESAFF hufanyakazi kwenye maeneo ya uwajibikaji kijamii ili kuboresha matumizi ya bajeti ya kilimo kwa kuhakikisha ushiriki wa wakulima wadogo kwenye mifumo ya bajeti ngazi za vijiji, kata wilaya hadi taifa – ikilenga wilaya zipatazo 32 kwenye ukanda huo. Wanachama wa ESAFF ni pamoja na Burundi (ESAFF Burundi), DRC Congo – FOPAC, Kenya – KESSFF, Lesotho – ESAFF Lesotho, Madagascar – CPM, Malawi – NASFAM, Mozambique – ROSA, Seychelles – SEYFA, South Africa – ESAFF South Africa, Swaziland – CIEAS, Rwanda – ESAFF Rwanda/APPPE, Tanzania – MVIWATA, Uganda – ESAFF Uganda, Zambia – ESAFF Zambia, Zimbabwe – ZIMSOFF.

## Kuhusu Kitini hiki cha Sera

Kitini hiki kimewezeshwa kupitia uhisani wa Trust Africa. Kimehaririwa na Bwana Audax Rukonge na mapitio yamefanywa na Bw. Stephen Ruvuga, Bw. Tom Laizer, Bw. Joe Mzinga na Bw. Anthony Muchoki.



*Kitini hiki kimetengenzwa kwa msaada wa Trust Africa. Maoni yaliyoko kwenye kitini hiki cha sera ni ya ESAFF na wanachama wake na kamwe hayawakilishi mtizamo rasmi wa wafadhili wetu*